

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA  
UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**

**01**

**KISWAHILI**

**Muda Saa 1:30**

**Mwaka: 2020**

**Maelekezo**

1. Mtihani huu una sehemu A, B, C, D na E zenye jumla ya maswali **matano (5)**.
2. Jibu maswali **yote** katika kila sehemu.
3. Sehemu A, B, C, D na E zina alama **kumi (10)** kila moja.

**SEHEMU A: (Alama 10)**

1. Sikiliza kwa makini sentensi zinazosomwa kisha uziandike kwa usahihi katika nafasi zilizoachwa wazi.
  - (i) \_\_\_\_\_
  - (ii) \_\_\_\_\_
  - (iii) \_\_\_\_\_
  - (iv) \_\_\_\_\_
  - (v) \_\_\_\_\_

**SEHEMU B (Alama 10)**

2. Katika kipengele (i) – (ii), andika herufi ya jibu lililo sahihi katika kisanduku.
  - (i) Neno “tumeimba” lipo katika hali gani?  
A. timilifu    B. iliyopita    C. iliyopo    D. ijayo    [    ]
  - (ii) Nilinunua matunda matamu. Neno “nilinunua” lipo katika wakati gani?  
A. Mtimilifu    B. Ujao    C. Uliopita    D. Uliopita    [    ]
  - (iii) Watoto \_\_\_\_\_ pilau juzi. Neno lipi kati ya maneno yafuatayo linakamilisha sentensi hii?  
A. watakula    B. wanakula    C. walikula    D. hula    [    ]
  - (iv) Neno lipi linaonesha wakati ujao kati ya maneno yafuatayo?  
A. Niliimba    B. Nitaimba    C. Huimba    D. Ninaimba    ]
  - (v) Mwaliimu \_\_\_\_\_ somo la Kiswahili sasa hivi.  
A. amefundisha    C. Hufundisha  
B. alifundisha    D. Anafundisha    [    ]

### SEHEMU C (Alama 10)

3. (i) Toa maana ya nahau zifuatazo kwa kuandika jibu lililo sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.
- (a) Kufa kishujaa \_\_\_\_\_
- (b) Kifungua mimba \_\_\_\_\_
- (c) Mkono wa birika \_\_\_\_\_
- (ii) Kamilisha methali zifuatazo kwa kuandika jibu lililo sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.
- (a) Maji yakimwagika \_\_\_\_\_
- (b) Fuata nyuki \_\_\_\_\_

### SEHEMU C (Alama 10)

4. Sentensi zifuatazo zimechanganywa, zipange katika mtiririko unaoleta maana kwa kuzipa herufi A, B, C, D na E. Sentensi ya (i) imetumika kama mffano.
- (i) Nikifika shuleni nitaanza masomo. **E**
- (ii) Kila siku ninaamka asubuhi. \_\_\_\_\_
- (iii) Kisha ninaondoka kwenda shuleni. \_\_\_\_\_
- (iv) Ninapiga mswaki na kuoga. \_\_\_\_\_
- (v) Dada ananipa chai na chapati. \_\_\_\_\_
- (vi) Ninakunywa chai na chapati. \_\_\_\_\_

### SEHEMU C (Alama 10)

5. Soma kwamakini kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata kwa kuandika jibu lililo sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

Yoya na Bura wanaishi katika kijiji cha Ulanga. Watoto hao walikuwa na tabia ya ukaidi. Kila walipoonywa na wazazi wao hawakutii. Walimu pia walitimiza wajibu wao wa malezi hivyo mara kwa mara waliwashauri kuacha tabia ya ukaidi. Japokuwa walionywa na walimu pamoja na wazazi lakini hawakubadilika.

Walipofika Darasa la Nne, watoto hao walianza tabia ya utoro na hatimaye waliacha shule. Walikubaliana kuanza biashara ya kuuza mkaa. Kila siku walikwenda msituni kukata miti kwa ajili ya kuchoma mkaa.

Wazazi wao waliwaonya kwa kuwakumbusha katazo la serikali kuhusu ukataji wa miti ovyo.

Siku moja walipokwenda kukata miti msitumi, viongozi wa serikali ya kijiji waliwavizia na kuwakamata. Walipelekwa kwenye ofisi ya kijiji. Huko walipata adhabu kali na kuamriwa kupanda miti ishirini kwa kila mmoja.

Walijutia ukaidi wao na kuomba radhi kwa wazazi na walimu wao. Walisamehewa na walirudi shuleni kuendelea na masomo. Toka wakati huo watoto hao walikuwa na heshima na watiifu sana.

**Maswali:**

- (a) Ni tabia gani mbaya walizokuwa nazo Yoya na Bura?
  - (i) \_\_\_\_\_
  - (ii) \_\_\_\_\_
- (b) Ni tabia gani iliwafanya Yoya na Bura kuacha shule? \_\_\_\_\_
- (c) Baada ya kupewa adhabu Yoya na Bura walifanya nini? \_\_\_\_\_
- (d) Habari hii inahusu nini? \_\_\_\_\_
- (e) Habari hii inakufundisha nini? \_\_\_\_\_